

**Dondoo za mkutano wa kwanza wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam.
Jumamosi 28 Januari 2006 Saa 3 asubuhi -6 mchana
Bustani mkabala na Palm Beach Hotel**

Waliohudhuria:

Jina	Makazi	Jina	Makazi
Abdallah Khatib	Magomeni	Mejah Mbuya	Mwenge
Ally Saidi		Moshi Matola	Matola
Ally Salum	Magomeni Mwembe Chai	Othman Makange	Kigamboni
Paulo Atibu	Keko Mwangi	Ramadhani	Tandale
Baunsa Aushaweji	Tandale	Ramadhani F	Magomeni Mwembe Chai
Chrisworny C. Msonga	Kinondoni	Ranji Ayoub	Magomeni Kagera
Elaine Baker	Magomeni Makuti	Said	Kikiaran
Faridi Biashala		Saidi	Manzese
Francis Michael	Kinondoni	Salum Abdalla	Tandale
Israel Kiyame	Tabata	Salum Chimburumbu	
John Emil Maximilian	Ilala	Salum Kambi	Kisiwani
Joseph Ngalowoka	Mwananyamala Kisiwani	Shukuru Hassan	Magomeni
Juma Ali Salehe Jongo	Manzese	Siyenu Mohammad Ramadhani	Tandale
Kibwana Mohammad Msiga	Vingunguti	Tendekayi Guni	Magomeni Makuti
Mandela Mashi	Tandale	Uwesu Rajabu	Mwananyamala
Maurus Malikita	Msasani		

Mkutano ulifanya kwa Kiswahili

Sababu za kuanzisha UWABA

Mejah Mbuya alitoa utangulizi kuhusu kuanzishwa kwa UWABA.

Kulikuwa na mjadala kuhusu sababu za kuanzishwa kwa UWABA. Hoja zilikuwa kama ifuatavyo:

- Wapanda baiskeli wanapata matatizo na ni kupitia ushirika tunaweza kuwa na sauti maoja na kutatua matatizo hayo.
- Tatizo kubwa ni Usalama barabarani. Sababu hasa za tatizo zinajumuisha uchache wa maeneo ya kuendeshea baiskeli, ukosefu waheshima wa madereva kwa wapanda baiskeli, wapanda baiskeli kutokuelewa haki zao na kutokujua sheria za barabarani.
- Tatizo jinngine ni kukosekana kwa vifaa vya kunawia mtu anapofika mwisho na kuwa na joto, ukosefu wa maegesho ya baiskeli na pia daladala hazina sehemu ya kubebea baiskeli.

Sababu nyingine ni

- Kushirikiana kuhusu taarifa za usalama.
- Kuwasaidia wapanda baiskeli waliopata ajali kupata haki zao.
- kuwahamasisha wengine hasas wanawake kuepanda baiskeli.
- Kuweka mtandao na wapanda baiskeli wengine ulimwenguni na kujihusisha kwenye mjadala/matukio kuhusu upandaji baiskeli kama mojawapo ya usafiri.

Maana ya baiskeli

Miongoni mwa waliohudhuria walikuwa wenye ulemavu watumiao baiskeli za mikono. Ilikubalika kuwa hata zijumuishwe kwenye maana ya baiskeli kwa UWABA. Nyongeza, baiskeli zitumiazo tairi mbili zinazobeba mizigo na bidhaa pia zijumuishwe.

Faida za matumizi ya baiskeli

Faida zilizadiliwa. Faida binafsi zinahusisha kufanya mazoezi, kufika mapema kuwapa na foleni, kuwa huru na kupunguza gharama. Faida za kimazingira na kijamii ni pamoja na kupunguza uchafuzi wa mazingira na msongamano barabarani. Upandaji baiskeli ni kitu cha kujivunia na si usafiri wa maskini.

Katiba

Mswada wa katiba ulijadiliwa na kusomwa. Kulikuwa na majadiliano na maelezo na pia madadiliko kidogo yalikubaliwa. Katiba ilipitishwa bila pingamizi kwa waliokuwepo.

Uchaguzi

Mejah Mbuya alipendekezwa kuwa mwenyekiti na hakuna mwingine aliyejitokeza. Ilikubalika awe mwenyekiti bila pingamizi.

Elaine Baker alipendekezwa kuwa katibu na hakuna mwingine aliyejitokeza. Ilikubalika bila pingamizi.

John Emil Maximilian alipendekezwa kuwa mweka hazina na hakuna mwingine aliyejitokeza. Ilikubalika bila pingamizi.

Kulikuwa na majadala kuhusu idadi ya wajumbe wa kamati wawe zaidi ya watano. Ila ilipendekezwa kuwepo na kamati nyingine ya muda ili kamati kuu ibaki kuwa na wajumbe watano. Ilikubalika kuwa wajumbe wengine wawili wangechaguliwa kwenye kikao kitakachofuata.

Fomu za Usajili na Ukaguzi

Fomu za usajili wa wajumbe zilisambazwa na kujazwa na kila mjumbe aliyekuwepo.

Mapitio ya hiari yalifanyika ili wajumbe wajaze maoni na kukusanya maelezo kwa wajumbe. Ilijazwa na idadi kubwa ya waliokuwepo.

Mawazo ya jinsi ya kuendelea

Ilipendekezwa kwamba tuwaambie wataalam wa sheria za barabarani au wanasheria kutupa maelezo kuhusu sheria za barabarani na haki za wapanda baiskeli.

Baada ya saa tatu kupita, ilikubalika kuwa mkutano mwingine uwe saa 3 asubuhi jumamosi itakayofuata sehemu hiihii.